

## **Sera ya utofauti na kupambana na ubaguzi ya idara ya taaluma za kiafrika**

1. Tunakubali kwamba sisi sote tumeathiriwa na upendeleo wetu wa jamii, marupurupu tunayo nayo au tunakosayo kwa ajili ya miundo na yanayohusika ubaguzi wa aina tofauti kama kwa mfano: rangi ya ngozi; pendekezo la kijinsia; dini; ulemavu; utaifa; jinsia; hadhi ya kijamii; umri; lugha, n.k.
2. Idara ya taaluma ya kiafrika inakusudia kuwa nafasi salama na kushughulikia maswali yoyote ya upendeleo, ubaguzi wowote na kumpa kila mmoja wakati wote nafasi ya kusoma na ya kufanya kazi kwa heshima.
3. Tunatetea ujumuishaji na usawa wa watu wote na kuepusha rangi ya ngozi; pendekezo la kijinsia; dini; ulemavu; utaifa; jinsia; hadhi ya kijamii; umri; lugha, n.k.
4. Tunakubali na Taarifa ya Ulimwengu juu ya Haki za Binadamu na haswa kuhakikisha kwamba lila mmoja ana haki ya uhuru wa kutoa na kueleza maoni yake (ona kifungu cha 19<sup>1</sup>).
5. Tunajitahidi kuhakikisha enzi kuu la watu wote wanaofanya kazi kwa idara yetu na wa wote wasiofanya kazi kwa idara na ambao wakabiliwa kwa ubaguzi au washuhudia ubaguzi.
6. Tunataka kushughulikia kesi zote za ubaguzi mdogo na mkubwa ya ndani na ikiwa ni lazima kuwashirikisha wataalamu na wanachama wa mashirika mengine wanaoshirikiana nasi (tazama).
7. Tunasaidia kuwezesha hatua kama zile za kutoa taarifa hadharani, hotuba za watu wote, semina, mafunzo kwa wao wanaofundisha, kupambana na ubaguzi.
8. Tumeanzisha utaratibu wa kutoa uwazi wa kushughulikia ubaguzi: taratibu za malalamiko na ushauri, uchunguzi, matokeao. Hatua zinazochaguliwa kwa msingi wa kila kesi.
9. Ikiwa mtu fulani aomba tunamhakikishia kila mtu anayehusika na ubaguzi kutokujulikana.
10. Tunahakikisha kuwa sera hii inapatikana hadharani na kwamba sera hii inaweza kutumiwa kwa madai ya ubaguzi.
11. Sera hii inapatikana kwa lugha zifuatazo: Kiswahili, Kibambara, IsiZulu, Kihausa, Kiarabu, Kijerumani, Kiingereza, na Kifaransa.

Tafsiriwa na Daniela Waldburger

---

<sup>1</sup> <https://www.ohchr.org/EN/UDHR/Pages/Language.aspx?LangID=swa>